HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

MPANGO WA USIMAMIZI WA MISITU

KIJIJI CHA MACHEMBA

MUHUTASARI

Utangulizi

Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998 inatoa kipaumbele kwa jamii kushirikishwa katika usimamizi wa misitu. Pia sera inasisitiza mchango wa sekta ya misitu katika kukuza kipato cha jamii ili kupunguza umasikini. Ufupisho huu unaelezea vipengele muhimu vya usimamizi wa msitu wa kijiji cha Machemba utakaotumika katika kipindi cha miaka mitano. Lengo la nikuwezesha kutoa uelewa wa haraka uliopo ndani ya mpango

Umiliki wa msitu

Msitu wa Chiumbe unamilikiwa na Serikali ya Kijiji cha Machemba. Msitu huu ulitengwa kuwa Msitu wa hifadhi wa kijiji cha Machemba mwaka 2007 chini ya usaidizi wa kitalaamu toka kwa wawezeshaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kwa ufadhili wa TASAF. Halmashauri ya wilaya ya Tunduru wakishirikiana na Shirika la MCDI, MJUMITA na WWF walimalizia mchakato wa Usimamizi Shirikishi wa Msitu kutoka ngazi ambayo iliachwa na wawezeshaji wa mwanzo na kumilikishwa kwa Serikali ya Kijiji cha Machemba mwaka 2015 baada ya mpango wa usimamizi na sheria ndogo za msitu kupitishwa na Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru.

Lengo kuu la Mpango wa usimamizi wa misitu

Msitu wa Kijiji ulitengwa kwa lengo la kuvuna mazao ya mbao, mazao timbao na rasilimali zingine za misitu kiendelevu. Lengo kuu likiwa ni kuweka msitu katika hali ya uasilia na kuboresha hali ya maisha ya kizazi kilichopo na kijacho.

Madhumuni

Kuboresha hali ya uhifadhi wa maliasili katika kijiji;

Kuhifadhi eneo lenye ukubwa wa hekta 4,612 la Msitu wa Kijiji cha Machemba kwa kudhibiti ukataji miti hovyo, uharibifu na matumizi yasiyofaa.

- Kuhakikisha kunakuwepo na upatikanaji wa mazao yasiyo timbao wakati wote kwa ajili ya matumizi ya kawaida.
- kuongeza mapato ya Kijiji kutokana na uvunaji endelevu wa rasilimali za misitu.
- Kuhifadhi na kulinda uoto wa asili wa msitu na bionuai kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho

Maelezo kuhusu Msitu

Msitu wa hifadhi wa Kijiji cha Machemba unaitwa Chiumbe

Mahali ulipo Msitu na ukubwa wake

Msitu wa hifadhi wa Chiumbe una ukubwa wa hekta 4,612 na upo upande wa Magharibi katika ardhi ya kijiji. Msitu huu unapakana kijiji cha Legeza mwendo upande wa Kaskazini na upande wa Mashariki Msitu huu unapakana na eneo la kilimo la kijiji cha Legeza mwendo, upande wa Kusini Msitu unapakana na Kijiji cha Mkandu na upande wa Magharibi msitu unapakana na Kijiji cha Mpanji.

Msitu unafikika kwa njia ya gari kupitia barabara inayoelekea katika Kijiji jirani cha Mpanji.

Jamii ya miti

Kuna aina nyingi za jamii tofauti za miti katika Msitu wa Kijiji. Jamii za miti ya mbao na ya thamani zilizopo Msituni ni Mninga jangwa/Mtumbati *(Pterocarpus angolensis)*,

Mkongo/Mbambakofi (*Afzelia quanzensis*), Mpingo *(Dalbergia melanoxylon)*, Mpangapanga/Mpande *(Milletia stuhlmannii)*, Mtondoro/Mpapa (*Julbernadia globiflora*), Mchenga (*Brachystegia speciformis*), Mkarati *(Burkea africana)*, Mjembe, Mteteleka, Mbuni, Mgelegele, Msechela, Msekeseke, Mgwina, Mpindimbi, Mtuanjiwa

Mazao yasiyo timbao

Kuna aina mbalimbali za mazao yasiyo timbao kama vile uyoga, asali, viazi pori madawa ya asili, kamba, miyaa na nyasi.

Miti ya matunda ni Mdawa, Ukwaju, Mbiinji, Ngangandembo, Ngungumwale, Matopetope, Ndongozimba, Nkuju, Vindogolya, Maja, Mpindimbi, Mbubudu na mingineyo

Miti inayotumika kutengenezea kamba ni Mijombo, Mchinji, Mnola, Mchenga na Mnemela

Jamii za uyoga zifuatazo zinazopatikana katika Msitu huu, Mangunguli, Nakambalakata, Nakajongolo, Uzinda, Uboowa, Chimwaga Nzanda, Makuluja, Utembo, Nyama, Mkakuni, Ntima wa mbunju, Utenga n.k.

Wanyama pori na jamii za mimea

Baadhi ya wanyama wanopatikana katika msitu wa hifadhi wa kijiji ni Sungura, Tandala, Paa, Nyati, Simba, Chui, Tembo, Nyani, Tumbili, Fisi, Kima, Mbwa mwitu, Ngolombwe, Mbawala, Towe, Nguruwe, Ngiri,Mbawe, Mbalapi, Nungunungu, Nenje, Mbunju, Kakakuona, Kiboko, Kobe, Mikuli, Ndonda, Kikui, Mbendu, Bweha, Kenge, Chatu, Njudi, Komba, Kinyonga, Gwida na Ngereng'ende n.k.

Pia jamii ya ndege wanopatikana katika msitu wa hifadhi wa kijiji wa Chiumbe ni; kanga, kwale, chiriku, njiwa, tipitipi, kororo, njegea-msitu, kinjochi, kukunungu, pelepe, pondopondo, Ngulaka, Ngurukulu, Chengo, Bundi, Nalumbapala, Kwikwi, Kipeta, Twitwitwi, Kichapi,Tondowele, Kindororo na Mwewe.

Maeneo ya Usimamizi

Msitu wa hifadhi wa Chiumbe umegawanyika katika maeneo madogo ya usimamizi matatu ambayo ni eneo la asilimia kumi (10%), eneo la uvunaji na eneo la utalii.

Eneo lenye ukubwa wa asilimia 10 ya Msitu mzima ambalo ni sawa na hekta **461.2** limetengwa kama eneo la uhifadhi tu na uvunaji wa mazao ya misitu hauruhusiwi kabisa katika eneo hili. Tathimini shirikishi ya rasilimali za Msitu haitafanyika katika eneo hili. Eneo hili limeoneshwa katika **kiambatisho A** kwa rangi ya kijani kwenye ramani ya Msitu wa Kijiji. Eneo hili lilichaguliwa kama eneo la uhifadhi kwa sababu lina uoto unaowakilisha hali halisi ya Msitu mzima, ni makazi na mazalia ya wanyama na kuna mifereji ya msimu iliyopita katika eneo hili. Pia eneo hili litatumika kama eneo la ufugaji nyuki wa kisasa kwa sababu ufugaji huu ni rafiki kwa mazingira na hauambatani na uvunaji wa miti wala uchomaji wa moto hovyo

Eneo dogo jingine lilitengwa ni eneo la Nambembele ambalo litatumika kwa ajili ya shughuli za kitalii. Eneo hili lina asili ya bonde ambapo ni makazi ya wanyama, lina ukubwa wa hekta 34 na halitatumika kwa ajili ya shughuli yoyote ya uvunaji.

Eneo lililobaki ni eneo la uvunaji ambapo miti ya mbao yenye thamani imefanyiwa tathimini na kuandaliwa mpango wa uvunaji endelevu. Uvunaji endelevu wa miti iliyofanyiwa tathimini utafanyika katika eneo hili kwa kufuata mpango wa uvunaji

ulioandaliwa. Hata hivyo uvunaji hauruhusiwi kufanyika ndani ya mita sitini kutoka kwenye kingo za mito iliyopo katika eneo hili.

Matumizi ya msingi

Wanajamii wa kijiji cha Machemba watakuwa na haki ya kuingia katika msitu wa jamii bila kibali kupata matumizi ya msingi ya kufanya matambiko, maji na kupita njia zinazofahamika, haki hii itahusu vijiji jirani piaWasio wakazi wa kijiji hawataruhusiwa katika maeneo ya kijadi bila uangalizi wa kamati ya Maliasili.

Matumizi huru ya msitu

Matumizi huru kwa wanakijiji wa Machemba yatakuwa kwa ajili ya mazao yasiyotimbao,kama asali ya nyuki wasiouma, uyoga, kuni, majengo, matundapori, madawa ya asili na kutundika mizinga, vyote hivyo vitapatiwa kibali maalum cha bure kutoka serikali ya kijiji.

Wasio wakazi wa kijiji cha Machemba wanaweza pia kuomba kibali toka serikali ya kijiji kutumia mazao yaliyotajwa hapo juu toka msitu wa kijiji. Kamati ya maliasili itakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa mazao ya msitu yanayotolewa bure yanatumiwa kiendelevu na hayamalizwi toka msitu wa jamii. Watumiaji wa nje ya kijiji wanaotaka kuvuna mazao haya kwa ajili ya biashara wanaweza kutozwa ushuru kama ilivyopangwa na Kamati ya Maliasili.

Shughuli zifuatazo zitatozwa ushuru na serikali ya kijiji.

- Kutembelea msitu kwa ajili ya mafunzo.
- Utafiti.
- Utalii msituni.

Mazao Yanayohitaji Vibali vya Uvunaji

Kabla ya kuvuna jamii yeyote ya miti iliyoorodheshwa, lazima tathmini ifanyike ili kubaini kiasi kilichopo na mpango wa uvunaji utatayarishwa. Tathmini ya kina itafanyika kufuatana na mwongozo wa Tathmini Shirikishi ya rasilimali za misiti wa Idara ya Misitu na Nyuki katika Wizara ya Maliasili na Utalii. Taarifa za Tathmini shirikishi zimeambatanishwa katika mpango huu. Tathmini shirikishi haitafanyika katika eneo lililotengwa Kwa ajili ya hifadhi (eneo la 10% la msitu).

Mpango wa uvunaji utaelezea namna kiwango cha uvunaji kilivyopatikana kutokana na matokeo ya tathmini na utabainisha ni kwa namna gani kiwango hicho ni endelevu. Mpango wa uvunaji ni lazima upitishwe na kamati ya maliasili na kuambatanishwa katika mpango huu.

Mazao mengine ya misitu

Mazao mengine yote yatalipiwa ushuru sawa na sheria ndogo ya kijiji husika ila ada hiyo isizidi viwango vya sheria mama.

Matumizi yasiyoruhusiwa ndani ya msitu

- Kilimo ndani ya Msitu
- Kukata kuni mbichi
- Kubangua asali
- Kutega wanyama
- Kuchimba mawe, mchanga au udongo kwa ajili ya biashara

- Uchakataji wa mbao na magogo kwa kutumia chainsaw
- Kuchuna magome ya miti kwa ajili ya mizinga ya kienyeiji
- Kulisha mifugo ndani ya Msitu
- Makazi ndani ya Msitu
- Uvunaji wa miti ya mbao ambayo haijafanyiwa tathimini ya uvunaji endelevu
- Uvunaji katika eneo la hifadhi (eneo la 10%) au katika maeneo muhimu ya kimila na jadi, pia chanzo cha maji - mita sitini kutoka kingo za mto.
- Kuchoma moto hovyo
- Uanzishwaji wa njia mpya zisizo rasmi ndani ya Msitu
- Uchomaji wa mkaa
- Uwindaji wa wanyama bila kibali.

Shughuli za Kuendeleza na Kutunza Msitu

Mikakati ya jumla ya kutunza na kuendeleza misitu pamoja na rasilimali zake imewekwa bayana. Mambo yatakayoangaliwa ni utunzaji wa misitu hii ili isiharibiwe dhidi ya kilimo na moto. Ulinzi wa msitu, kinga na uthibiti wa moto pamoja na mpango wa matumizi endelevu wa mazao ya msitu utazingatiwa.

Usimamizi wa msitu wa kijiji utakuwa chini ya serikali ya kijiji na utatunzwa na wanajamii wote. Msitu utalindwa na jamii kuzingatia mipaka yake, kila mtu atatoa taarifa kwa uongozi wa kijiji au kamati ya maliasili au kikosi cha doria pale anapoona uharibifu katika msitu. Kamati ya maliasili itaratibu na kusimamia shughuli za doria.

Kutakuwa na timu ya doria itakayochaguliwa na mkutano mkuu wa kijiji ambayo itakuwa na jukumu la kufanya doria za mara kwa mara katika msitu wa jamii.

Vyanzo vya mapato

- Kurina asali;
- Kutembelea Msitu kwa ajili ya mafunzo;
- Utafiti,
- Utalii Msituni.

Mgawanyo wa mapato yatokanayo na mazao ya Msitu utakuwa kati ya Kamati ya Maliasili, Halmashauri ya Kijiji na Halmashauri ya Wilaya. Mgawanyo huu utazingatia nani mwenye majukumu makubwa zaidi katika kutunza na kuendeleza Msitu.

i) Kila mwaka Halmashauri ya Kijiji itatoa kiasi cha asilimia tano **(5%)** ya mapato yatokanayo na rasilimali za misitu kwa Halmashauri ya Wilaya kulingana na huduma ambazo Halmashauri inatoa.

ii) Asilimia thelathini **(30%)** ya mapato yatakuwa kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa Msitu chini ya Kamati ya Maliasili ya Kijiji. Sehemu ya mapato haya inaweza kutumika kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya kijiji kama mkutano mkuu wa kijiji ukiidhinisha hivyo.

iii) Asilimia sitini na tano **(65%)** iliyobaki itaenda kwa Halmashauri ya Kijiji kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo ya jamii.

Matumizi ya mapato

Mapato yatokanayo na msitu yataelekezwa katika shughuli za kuendeleza shughuli za msitu zilizopangwa katika mpango kazi wa mwaka. Mapato yatakayobaki yatapelekwa kwa serikali ya kijiji ili yatumike katika shughuli za jamii.

Matumizi halali ya mapato yatokanayo na msitu wa jamii ni:

- Kulipa motisha (posho) kwa doria.
- Kununuavifaa muhimu kwa ajili ya kuendeleza shughuli za msitu kama ilivyobainishwa katika mpango kazi wa mwaka.
- Matumizi mengine ya ziada ya kuendeleza msitu yaliyoidhinishwa na Serikali ya Kijiji.
- Ununuzi wa vitabu kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za shughuli za msitu.
- Kuchangia katika shughuli za maendeleo kijijini.

Usimamizi wa Fedha

Fedha zote zitatunzwa benki isipokuwa kwa fedha chache kwa ajili ya matumizi madogomadogo. Fedha ndogondogo hazitakiwi kuzidi shilingi 100,000/= Kutakuwa na akaunti benki itakayofunguliwa kwa jina la **Akauti ya Maliasili ya Kijiji cha Machemba** na itakuwa na watia sahihi

Taarifa ya Mapato na Matumizi

Kamati ya Maliasili itatoa taarifa ya Mapato na Matumizi kila mwezi kwa Serikali ya Kijiji na kila baada ya miezi mitatu kwa mkutano mkuu wa kijiji.

Kuwajibishwa

Mwanakamati au mwanakijiji yeyote atakayepatikana na kosa la kutumia vibaya fedha za msitu atawajibishwa na serikali ya kijiji au atashitakiwa katika Baraza la usuluhishi la kata au Mahakama ya mwanzo. Mjumbe yeyote wa Kamati ya Maliasili atakayepatikana na kosa lazima ajiuzulu haraka na nafasi iliyoachwa wazi ijazwe kufuata utaratibu unaokubalika.

Ufuatiliaji

Serikali ya Kijiji itafuatilia shughuli zote zilizopangwa kulingana na mpango kazi wa kila mwaka katika kipindi chote cha miaka mitano. Ufuatiliaji huu utahakikisha kuwa shughuli zote zimefanyika kulingana na mpango kazi.

Kiambatanisho A

Ramani inayoonyesha Mipaka ya Msitu wa Kijiji


Msitu wa kijiji cha Machemba (Chiumbe)
Hekta 4,612
286000
288000
290000
292000
8772000
8770000
8768000
8766000
8764000
8762000
Mto Msinjewa
Eneo la Kilimo
Kijiji cha Mpanji
Kijiji cha Mkendu
Ufunguo
Kona za mipaka
mto midogo
barabara
Eneo la Utalii (Nam'bembele)
Eneo la uhifadhi (as ilimia kumi)
Eneo la Uvunaji
N
W
E
S
2
1
0
2
Kilomita